**WIZARA YA ELIMU SAYANSI, TEKNOLOJIA NA MAFUNZO YA UFUNDI**



## SHULE YA MSINGI MARTIN LUTHER

**S. L. P 1786 Dodoma. Simu. +255 26 2395029, +255 784 449098**
**Fax +255 26 2395030 (www.martinlutherschooldodoma.com)**

***"Quality Education for the New Generation"***

---

# DARASA IV – KAZI YA NYUMBANI

# KISWAHILI

**JINA LA MWANAFUNZI: ______________________**

## MAELEKEZO

1. **Kumbuka kuandika majina yako matatu kwa usahihi.**
2. **Jibu maswali yoe kulingana na maelekezo.**
3. **Soma maswali kwa ufasaha kabla ya kuyajibu.**

**SEHEMU "A" : MATUMIZI YA LUGHA**

1. .Katika neno **KARATA** ukidondosha silabi moja ya kati utapata neno gani?
   A. Kara B. Kataa C. Kata D. Karata [ ]

2 .Bibi huwa habebi mizigo mizito sentensi hii ipo katika ukanushi wa wakati gani?
   A. Mazoea B. Timilifu C. Uliopo D. Uliopita [ ]

3. Kitendo cha jua kuzama upande wa Magharibi huitwaje?
   A. Mawio B. Mapambazuko C. Macheo D. Machweo [ ]

4. Andika wingi wa sentensi hii "Peni yangu imepotea"...................................
   A. Peni zetu zimepotea B. Peni yangu imepotea
   C. Mapeni yangu yamepotea D. Peni imepotea [ ]

5. Neno **TAMBIKA** ni kitenzi, ukibadili neno hili kuwa Nomino litakuwa ................
   A. Mtambika B. Tambiko C. Tambarika D. Tambi [ ]

6. Kinyue cha neno **KUBWA** ni ......... A. fupi B. nyembamba C. chache D. ndogo [ ]

7. Kanusha sentensi isemayo " Mariam anasoma kitabu"............................................
   A. Mariam ni mtaalamu wa kusoma kitabu B. Mariam hasomi kitabu
   C. Mariamu hasomi vitabu D. Mariam atasoma kitabu [ ]

8. Nomino inayotokana na kitenzi **IMBA** ni .................
   A. imbika B. imbiwa C. wimbo D. imba [ ]

9. Nyumba ya ndege inaitwaje? A. kiota B. kichungu C. banda D. msituni [ ]

10. Neno **KINDUMBWENDUMBWE** lina silabi ngapi?
    A. kumi na sita B. nane D. tatu E. tano [ ]

11. **Kanchiri** huvaliwa sehemu gani ya mwili? ..................................
    A. kichwani B. kifuani C. kiunoni D. mikononi [ ]

12. Kinyume cha neno **"kichalichali"** ni ..................
    A. kifudifudi B. uso kwa uso C. kichefuchefu D. kimgongomgongo [ ]

13. Mzee Kenge alimwekea .....................mtuhumiwa katika kituo cha polisi.
    A. zamana B. thamana C. samana D. dhamana [ ]

14. "Mhunzi" ni mtu anaye .......................
    A. fua nguo B. lina asali C. fua vyuma D . fua dhahabu [ ]

15. Mtu asiye na pua huitwa ...........A. kibwengo B. toinyo C. kigego D. kiokote [ ]

16. Kinyume cha neno rejea ni: A. Rudia B. Nenda C.Rudi D. Subiria [ ]

17. Kabati, meza, kitanda, kiti na dawati kwa jina moja hujulikana kama:
A. Thamani B. Samani C. Shule D. Darasa [ ]

18. Umoja wa neno maendeleo ni:
A. Muendeleo B. Endeleo C. Maendeleo D. Mwenendo [ ]

19. Silabi ipi katika neno **tuliwasubiri** inaonesha wakati?
A. Tu- B. -ri- C. –wali- D. –li- [ ]

20. Baba aliniambia nimwandikie ________ ya vitu ninavyohitaji kwa ajili ya shule.
A. Orodha B. Orotha C. Oroza D. Olodha [ ]

21. Vina, mizani, mshororo, ubeti na kibwagizo ni vipengele muhimu vya nini?
A. Mawasiliano B. Mashairi C. Habari D. Barua [ ]

22. Viimbo vya lugha ya Kiswahili ni vipi kati ya hivi vifuatavyo?
A. Mshangao, amri, maelezo, maulizo B. Maelezo, sauti, amri, maulizo
C. Amri, kusoma, mshangao, maelezo D. maulizo, nyimbo, maelezo, amri [ ]

23. Ni nini maana ya nahau hii "KATA UHUSIANO".
A. Habari ujamaa B. Maliza uwezo C. Ondoa ndugu D. Vunja urafiki [ ]

24. Ukibadili **NOMINO** iitwayo **SHUTUMA** utapata **KITENZI** gani?
A. Shutuma B. Shutu C. Shutumu D. Shutum [ ]

25. Jua huchomoza kutoka upande gani?
A. Magharibi B. Mashariki C. Kusini D. Kaskazini [ ]

26. Kamwe __________ Darasa la nne.
A. Nitarudia B. sitarudia C. Ningerudia D. ningependa [ ]

27. Nilipatwa na ______ baada ya kufaulu mitihani.
A. Furaha C. majonzi B. Machozi D. majonzi [ ]

28. Jina jingine la fanicha " ni ________
A. Sahani C. thamani B. samani D. Vitu vya ndani [ ]

29. Kitendo cha "kuvuna asali" huitwa ________
A. Kupakua C. Kuchota B. Kurina D. Kumimina [ ]

30. Wazazi wangu waliniandalia ______fupi baada ya kufaulu mitihani.
A. Sikukuu B. tafrija C. Kalamu D. rambi rambi [ ]

31. ......................makubwa huingiza hewa na mwanga wa kutosha.
A. kabati B. madirisha C. chumba D. ufa [ ]

32. Niliumia usoni baada ya kujigonga. A. ukutani B. ulizo C. mikono D. mwari [ ]

33. Tumekula chakula ..........mchana. A. ya B. za C. cha D. wa [ ]

34. Huu ni .............wa shule yetu na kijiji. A. mtani B. maringo C. giza D. mpaka [ ]

35. Samson ametengeneza .............ya chakula. A. vyoo B. meza C. unga D. moto [ ]

36. Viatu ...............baba vinang'aa. A. vya B. ya C. la D. wa [ ]

37. Ukitazama ............ utajua leo ni siku gani ya wiki.
A. jua B. mwezi C. kalenda D. giza [ ]

38. Mtu mwenye ..................nzuri ataajiriwa kuwa Afisa mtendaji wa kijiji.
A. wizi B. uchoyo C. michezo D. sifa [ ]

39. Tulichuma machungwa na kuyahifadhi ndani ya ................
A. gunia B. mkate C. shuka D. sauti [ ]

40. ............yake wa kwanza anaitwa Mariam. A. mvulana B. mzee C. binti D. mzigo [ ]

41. Bibi yangu ni ............ wa vyakula vya sherehe.
A. mpishi B. mkanyagaji C. mropokaji D. anayejenga [ ]

42. Hebu .............kusimulia hadithi hiyo maana ni nzuri mno.
A. leta B. rudia C. kamata D. paka [ ]

**SEHEMU "B": LUGHA YA KIFASIHI.**

***Chagua maana za Nahau, Methali na Vitendawili vifuatavyo.***

43. Piga chenga ni ................
A. pata chenga B. kuchenga C. kukwepa D. kucheka [ ]

44. Kula kiapo ni ..............A. kuahidi B. kula epo C. kuongea D. kuchenga [ ]

45. Kula chumvi nyingi ni ......................
A. kulamba chumvi B. kubugia chumvi C. ishi miaka mingi D. ishi maish mafupi [ ]

46. Kulia kwake, ni kicheko kwetu.............. A. mbwa B. mvua C. chura D. paka [ ]

47. Kuuliza ................ A. ni ujinga B. kupoteza muda C. si ujinga D. ni ahadi [ ]

48. Timu yetu ilishika mkia.***Shika mkia*** ina maana gani?
A. Kuongoza B. Kuwa ya mwisho C. Kushika usukani D. Kufanya vizuri [ ]

49. Malizia methali hii: Ngoja ngoja ......................................
A. Kusubiri sana B. Kuvuta heri
C. huumiza matumbo D. Huleta uvumilivu [ ]

50. Kilemba chake hatui wala haazimishi. Jibu la kitendawili hiki ni ................................
A. Jogoo B. Bibi kizee C. Jongoo D. Nywele [ ]

51. Methali gani inatutaka tusichoke na kukata tamaa? ......................................
A. Mchagua jembe si mkulima B. Mvumilivu hula mbivu
C. Kuishi kwingi kuona mengi D. Wingi si hoja [ ]

52. Piga hodi maana yake ni .........
A. kulipa kodi B. piga oni C. piga hodi D. kuomba ufunguliwe [ ]

53. Mchagua jembe ......A. si mkulima B. ni mkulima C. hulima D. hujua sana [ ]

54. Nyumba yangu haina mlango. Jibu lake ni ..........
A. ghorofa B. chumba C. yai D. kiberiti [ ]

55. Aga dunia. Maana yake ni .............
A. kuipungia dunia B. fariki C. kupoteza dunia D. kuipenda dunia [ ]

56. Mwenda pole .......... A. anaanguka B. ni mjinga C. ni mpole D. hajikwai [ ]

57. Kamilisha methali hii, "baniani mbaya................................................."

58. Nini maana ya nahau, **ficha makucha**..................................................

59. Tegua kitandawili hiki, **Masikini huyu hata umchangie vipi haridhiki**.........................................................................................

60. Ni methali gani inafaa kwa mtu ambaye anazikana mila, desturi na tabia zake asilia na kufuata za watu wengine...................................................................

61. Nahau isemayo **ana mkono wa birika** ina maana kuwa................................

**SEHEMU" C": UTUNGAJI**

**(i) Kamilisha barua ifuatayo kwa kuchagua maneno sahihi kutoka kwenye kisanduku kasha uyajaze sehemu zilizoachwa wazi.**

| |
|---|
| Kutoka, dhumuni la , madhumuni ya, mpendwa, S.L.P 670, wapendwa, kuhitimu, kuanza, S.L.P.,kurejea |

Shule ya Msingi Umoja,

(62)..................

Hendeni – Tanga.

**6 Mei, 2019.**

(63) ...................................baba na mama,

Salaam nyingi ziwafikie huko mliko nikitumaini ya kwamba wote hamjambo na mnaendelea vizuri na majukumu yenu. Mimi pia ni buheri wa afya na ninaendelea vizuri na masomo yangu.

(64) .......................................barua hii ni kuwajulisha kwamba, mwezi ujao tutapata likizo ndefu ya (65) .........................................muhula wa kwanza wa masomo, hivyo nitatakiwa (66) ............................nyumbani kwa ajili ya mapumziko.

Nitafurahi sana kuja kujumuika nanyi katika kipindi hicho cha likizo.

Nisalimie wadogo zangu Suzi na Baraka.

Mtoto wenu mpendwa,

**Mariam.**

**(ii) Panga sentensi zifuatazo ili zilete mtiririko unaofaa kwa kuzipa herufi A,B,C,D, E**

67. Kumbe basi hilo ndilo alilosafiria rafiki yangu. [ ]
68. Kulipopambazuka nilioga harakaharaka nikavaa upesi na kuelekea kituo cha mabasi [ ]
69. Baada ya kuangaza huko na huko nikaona basi la kwanza likiingia pale kituoni [ ]
70. Aliposhuka nikamlaki kwa kufurahi na kuelekea naye nyumbani [ ]
71. Ingawaje sikuchelewa lakini nilijawa na wasiwasi pale kituoni [ ]

**(iii) Panga sentensi zifuatazo ili zilete mtiririko unaofaa kwa kuzipa herufi A,B,C,D, E**

72. Ndege wote waliishi kijiji kimoja [ ]

73. Ndege wote walihudhuria mkutano huo [ ]

74. Mwenyekiti wao alikua mbuni [ ]

75. Hapo zamani za kale, [ ]

76. Siku moja aliitisha mkutano mkubwa. [ ]

***(iv) Jaza nafasi zilizoachwa wazi kwa kuchagua jibu lililo sahihi kutoka katika kisanduku kifuatacho.***

| |
|---|
| **Kisogo, ulimi, mvua, macho, meno, poteza matumaini, kukubali jambo, kuumia moyo, barafu** |

77. Nahau “vunja moyo” maana yake ni ipi? .........................................................................................

78. Kitendawili kisemacho “mjomba hataki tuonane” jibu lake ni lipi?

.........................................................................................................................................................

79. Nahau “unga mkono” maana yake ni ipi?

.........................................................................................................................................................

80. Kitendawili kisemacho, Popoo mbili zavuka mto, jibu lake ni..................................................

81. Nina saa yangu tangu ilipowekwa ufunguo haijawahi kusimama, jibu la kitendawili hiki ni....................................................

**SEHEMU “D”: SHAIRI**
***Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata kwa kuandika jibu sahihi.***

A. Kazi zote Duniani, namba wani mkulima,
Anapita kila fani, hata kama hakusoma,
Kula haendi sokoni, au kuomba kama Juma,
Zunguka Dunia nzima, kazi bora ni kilimo.

B. Kilimo ni mkombozi, kinga ya umaskini,
Humpa mtu makazi, mavazi na burudani,
Pato lake si la mwezi, posho haikosi ndani,
Zunguka Dunia nzima, kazi bora ni kilimo.

C. Lima pamba au buni, mahindi na maharage,
Pamoja tunza nyumbani, japo punje usimwage,
Ukipeleka sokoni, utapanda hata ndege,
Zunguka Dunia nzima, kazi bora ni kilimo.

D. Ulime kiendelevu, au jembe la mkono,
Usipokuwa mvivu, njaa hukupa mkono,
Utaishi kishupavu, na pia kwa majivuno,
Zunguka Dunia nzima, kazi bora ni kilimo.

**MASWALI.**

82. Mtunzi wa shairi hili anahimiza kuhusu nini?

Anahimiza kuhusu ……………………………………………………………………

83. Ni zao gani limetajwa kwenye shairi ambalo hutumika kama mboga?

…………………………………………………………………………………………

84. Ni wapi ukizunguka utabaini kwamba kazi bora ni kilimo? …………………………………

85. Shairi hili lina beti ngapi? ……………………………………………………………………

86. Mwandishi anasema kilimo ni kinga ya nini? ……………………………………………………

**SEHEMU E: UFAHAMU:**

***(i) Soma habari ifuatayo kisha jibu maswali.***

Mkulima ni mtu muhimu sana katika nchi yetu. Mkulima ndiye anayelima mazao mbalimbali ambayo yanasaidia kuondoa baa la njaa. Taifa likikumbwa na baa la njaa mambo yafuatayo hutokea . kwanza watu hukosa nguvu za kufanya kazi mbalimbali za ujenzi wa Taifa, kisha vifo vingi hutokea.

**Maswali.**

87. Bila mkulima nchi inaweza kupata ......................la njaa.

88. Nchi ikikumbwa na tatizo la njaa watu wake hukosa ...................za kufanya kazi mbalimbali za ujenzi wa Taifa.

89. Njaa haina mchezo inaweza kusababisha .......................vya watu.

90. Mwandishi anatueleza kuwa mkulima ni mtu ..............sana katika nchi yetu.

***(ii)* Soma habari ifuatayo kwa umakini kisha jibu maswali**.

Yohana ni mtoto wa kwanza katika familia ya Bwana na Bibi Daudi, ana wadogo zake wawili ambao ni Ansila na Amosi. Familia hii imejaliwa sana kuwa na mali nyingi kutokana na ukulima, biashara na ufugaji ambao bwana na Bibi Daudi wanauendesha. Mwaka uliopita Yohana alikuwa darasa la nne, Ansila darasa la pili na Amosi alikuwa bado hajanza shule.

Familia hii inaishi maisha ya **ukwasi.** Hivyo wanakijiji wengi wasio na mbele wala nyuma hupenda kuenda kuomba msaada wa chakula na fedha kwao. Wanapofika hupokelewa kwa mikono miwili na hufurahia sana maisha ya familia hii, Ama kweli kutoa ni moyo.

**MASWALI:**

91. Nini maana ya ukwasi?_______________________________________________

92. Familia hii ina jumla ya watu wangapi?____________________________________

93. Bwana na bibi Daudi wanajishughulisha na nini?______________________________
**Taja shughuli moja tu**

94. **Kifungua Mimba** katika familia hii ni ____________na **mziwanda** ni_____________

95. Unafiriki mwaka huu Yohana atakuwa darasa la ngapi?___________________________

***(iii)Soma kifungu cha habari kwa makini kasha jibu maswali***

Mimi ninaitwa Jack. Ni mtoto wa pili kuzaliwa katika familia yetu. Ninasoma darasa la nne katika shule ya Msingi Zilipendwa. Baba yangu ni Daudi na mama yangu ni Kigagu. Dada yangu anaitwa Mdoli na kaka yangu anaitwa Kihiyo. Mdoli yuko mbele yangu kwa madarasa mawili. Kihiyo bado hajaanza kusoma kwa kuwa yeye bado ni mdogo.

**MASWALI.**

96. Familia hii ina jumla ya watu wangapi? ......................
    A. Tatu B. Sita C. Wanne D. Watano [ ]

97. Mtoto wa kwanza kuzaliwa katika familia hii anaitwa nani?..........................
    A. Jack B. Mdoli C. Kihiyo D. Daudi [ ]

98. Mdoli anasoma darasa la ...............................
    A. Kwanza B. Tano C. Sita D. Nne [ ]

99. Jack anasoma darasa la ngapi? ................................ A. 7 B. 3 C.4 D. 10 [ ]

100. Baba yake Jack anaitwa Daudi, Je mama Mdoli anaitwa nani?
    A. Kokundya B.Mdoli C.Babu. D.Kigagu [ ]

**"Elimu ni uzima wangu" (Methali 4:13)**



MARTIN LUTHER SCHOOL